

# Wanafunzi wa <sup>Pg 29</sup> kike wazungumzia maisha ya 'geto'

Tumaini Msowoya, Mwananchi  
tmsowoya@mwananchi.co.tz

Bahi. Maisha ya kupanga vyumba mitaani waliyo nayo wanafunzi wa kike wanaosoma katika shule mbalimbali za sekondari wilayani Bahi mkoani Dodoma, yamewachosha na sasa wamepaza sauti.

Kutokana na hali hiyo, wanafunzi hao wameiomba Serikali kuwajengea hosteli.

Wamesema maisha ya kupanga vyumba mtaani maarufu geto yanachangia kwa kiasi kikubwa utoro na ongezeko la mimba kutokana na vishawishi wanavyopata kutoka kwa baadhi ya wanaume.

Mwanafunzi wa kidato cha nne katika Sekondari ya Magaga, Mlekwa Matonya alisema wapo wenzao walioshindwa kuendelea na masomo kutokana kuishi kwenye vyumba walivyopanga. "Wengi tunapata mlo mmoja kwa siku na wengine wanakosa kabisa chakula. Hali hii si nzuri kwetu, ndio maana tunaomba tujengewe hosteli shuleni," alisema.

Asha Abdallah wa kidato cha kwanza katika shule hiyo, alisema kuna wakati wanaume hujaa nje ya vyumba vyao kupiga soga wakiwavizia, jambo linalotishia kujiingiza kwenye vitendo vya mapenzi wakiwa na umri mdogo.

Mwanafunzi wa Sekondari ya Chikopelo, Veronika Tito alisema licha ya shule yao kuwa na hosteli wanafunzi wengi wamepanga mitaani baada ya wazazi wao kukosa fedha za kuwalipia. "Tunaomba tuondolewe gharama za hosteli, mzazi wangu hana uwezo ndiyo maana naishi ghetu," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magaga kilicho na wanafunzi wengi waliopanga mitaani, Laurent John alisema wengi wanaishi kwenye mazingira magumu kutokana na kuwepo wanaume wenye nia ya kuwaharibia masomo yao.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Uhuru katika Kijiji cha Chifutuka, Musa Kawayu alisema uhaba wa hosteli umewafanya wasichana wengi kuacha masomo. Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Elizabeth Kitundu alisema wapo kwenye mkakati wa kuhakikisha hosteli inajengwa.